JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

## MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA (TACAF)

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

# HUDUMA ZA MFUKO

## UTANGULIZI

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umeanzishwa kwa Sheria ya ujumuisho wa wadhamini (Trustees' Incorporation Act) 2002 (CAP. 318 R.E. 2023) na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 Septemba, 2020.

## LENGO LA MFUKO

Kuwezesha wadau wa sekta za utamaduni na sanaa ili wazalishe kazi bora zitakazoshindana katika soko la kitaifa na kimataifa, kujiendesha kibiashara kuzalisha ajira pamoja na kuchangia pato la Taifa.

.

## DIRA

Kuwa Mfuko madhubuti wa kukuza na kuendeleza ubora wa kazi za utamaduni na sanaa kwa maendeleo ya Taifa.

## DHIMA

Kuratibu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kazi za utamaduni na sanaa ili kuwezesha kazi hizo kukidhi viwango vya mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

## WALENGWA WA MFUKO

a) Vikundi vya Utamaduni na Sanaa;
b) Vyama vya Utamaduni na Sanaa;
c) Mashirikisho ya Utamaduni na Sanaa;
d) Makampuni yanayojishughulisha na Utamaduni & Sanaa;
e) Vituo vya elimu na mafunzo yanayohusiana na Utamaduni na Sanaa; na
f) Asasi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya Utamaduni na Sanaa.

## SEKTA ZINAZO HUDUMIWA NA MFUKO

**Mfuko unatoa huduma kwa sekta zifutazo:-**

- Sanaa za maonesho - ushereheshaji, ngoma, sarakasi, mapambo, upishi n.k;
- Sanaa za ufundi – uchongaji, uchoraji, urembo, uchapishaji, mitindo na mavazi n.k;
- Filamu – makala jongefu, filamu ndefu, filamu fupi n.k;
- Muziki - singeli, injili, kaswida, rege, kizazi kipya, dansi, taarabu, rhumba
- Lugha na fasihi – riwaya, tamthiliya, waghani, ushairi; na
  Uhifadhi na Urithi wa Utamaduni na Sanaa - kumbukumbu za amali za utamaduni, vituo vya urithi wa utamaduni na sanaa (Arts Gallery).

## HUDUMA ZA MFUKO

Mfuko unatoa huduma kuu tatu ambazo ni huduma za fedha, Mafunzo na Ushauri wa Biashara na Masoko & TEHAMA. Ufafanuzi wa huduma hizo ni kama ifuatavyo:-

| NA | HUDUMA | AINA YA HUDUMA |
|---|---|---|
| 1. | Huduma za Fedha | a) Mikopo<br>■ Mikopo ya Uendeshaji;<br>■ Mikopo ya Vifaa;<br>■ Mikopo ya Dharura; na<br>■ Mikopo ya Mikataba. |
| | | b) Uunganishwaji wa Huduma za Mikopo na Taasisi za Fedha |
| | | c) Ruzuku |
| 2. | Mafunzo na Ushauri wa Biashara | a) Mafunzo ya Urasimishaji wa Biashara<br>b) Mafunzo ya Ujuzi<br>c) Ushauri wa Biashara<br>d) Uandishi wa maandiko ya biashara/miradi |
| 3. | Masoko na TEHAMA | a) Maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa<br>b) Kuandaa Katalogi ya Bidhaa na Huduma za Sanaa na kuzitangaza kwa wadau<br>c) Kuwezesha uandaaji na matumizi ya Teknolojia za Kisasa za kutangaza bidhaa |

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

## HUDUMA ZA MIKOPO

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania unatoa aina nne za mikopo kwa wadau wa Utamaduni na Sanaa Tanzania kama ifuatvyo:-

| NA | AINA ZA MIKOPO | MADHUMUNI YA MIKOPO |
|---|---|---|
| 1. | Mikopo ya uendeshaji | Kuendesha kazi za walengwa kama vile matamasha, mashindano, kutayarisha au kuzindua kazi za utamaduni au sanaa na shughuli nyingine zinazofanana na hizo |
| 2. | Mikopo ya Vifaa | Kununua vitendeakazi vitakavyotumika katika kuzalisha kazi za utamaduni au sanaa |
| 3. | Mikopo ya kujikimu / Dharura | Mikopo ya muda mfupi kwa ajili ya kujikimu wakati wa safari za kuandaa au kufanikisha kazi za utamaduni au sanaa |
| 4. | Mikopo ya mikataba | Kuwezesha utekelezaji wa mikataba ya kazi za sanaa kwa wazabuni waliopewa kazi na wadau |

## HUDUMA ZA MAFUNZO NA USHAURI WA BIASHARA

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**Mfuko unatoa mafunzo katika maeneo yafuatayo:-**

**a) Mafunzo ya Urasimishaji wa Biashara**

Mfuko hutoa mafunzo ya umuhimu na urasimishaji wa biashara kwa wasanii pamoja na kuwaunganisha na mamlaka mbalimbali zinazohusika na Urasimi shaji wa Kazi, Biashara, Huduma na Bidhaa.

**b) Mafunzo ya Ujuzi**

Mfuko unaratibu utoaji elimu ya Ujuzi kwa wasanii kwa lengo la kuboresha Ushiriki wao kwenye shughuli za kiuchumi nchini Tanzania. Mafunzo haya husaidia kuwezesha njia mbadala za elimu, ajira, kujiajiri na ujasiriamali kwa vijana wanaofanya kazi za Sanaa au wanahitaji kujihususha na shughuli za Sanaa.

**c) Ushauri wa Biashara**

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania hutoa huduma za ushauri kuhusu ushindani wa kibiashara kwa Wazalishaji, Wafanyabiashara na Wadau Wengine katika eneo la Utamaduni na Sanaa ili waweze kukidhi sifa na viwango na mahitaji ya masoko la ndani na nje ya nchi. Ushauri unaotolewa kutumika kama nyenzo, ikiwa ni pamoja na upanganji wa biashara, uuzaji, uendeshaji biashara, usimamizi wa fedha, na marejeleo ya mikopo ya biashara.

Aidha, huduma hii hutolewa kwa simu, kumtembelea mteja katika mazingira yake ya biashara au kupitia njia zozote zitakazoonekana zinafaa.

**d) Uandishi wa Maandiko ya Biashara/Miradi**

Mfuko hutoa huduma za uandishi wa maandiko ya mradi/biashara kwa wadau wa Utamaduni na Sanaa kwa gharama nafuu.

## MASOKO

**Katika eneo hili Mfuko unatekeleza yafuatayo:-**

**a) Maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa**

Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania hufanya maonesho ya Kitaifa ya bidhaa za Utamaduni na Utamaduni na Sanaa mara moja kwa mwaka. Aidha, kupitia maonesho haya wasanii na wadau wengine hupata fursa ya kuuza bidhaa zao, kutamblisha bidhaa kwa jamii pamoja na kubadilisha uzoefu wa ujuzi wa biashara na bidhaa baina yao.Maonesho haya hushirikisha nchi ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki

Kwa upande mwingine, Mfuko hudhamini ushiriki wa wasanii katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kutambulisha bidhaa zao na kujifunza mbinu mbalimbali za kibiashara.

**b) Katalogi ya Bidhaa na Huduma za Sanaa**

Mfuko umeandaa orodha ya huduma na bidhaa za Sanaa inayoainisha watoa huduma au wazalishaji wake ili kuwaunganisha na masoko ya ndani na nje ya nchi. Katalogi hii inapatokana katika Tovuti ya Mfuko

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**Unaweza kupata taarifa za Mfuko kupitia maeneo yafuatayo:-**

a) Kupitia matawi yote ya Benki ya NBC na Benki ya CRDB nchi nzima
b) Maafisa Utamaduni walioko katika ngazi za Halmashauri na Mikoa;
c) Kupitia Ofisi zake zilizopo Jengo la Utumishi, Kivukono - Dar Es Salaam
d) Kupitia Tovuti; www.tacaf.go.tz; Mitandao ya kijamii; *mfukotamadunitz*

MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

Jengo la Utumishi,
Kitalu A, 8 Barabara ya Kivukoni,
11101 Kivukoni, Dar es Salaam.

0738 246 286/ 0738 246 315

www.tacaf.go.tz

mfuko.utamaduni@michezo.go.tz

mfukotamadunitz